# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

## *Cheti cha Ithibati*

Na. 1496

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

ISBN: 978-9912-9923-6-8

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 27 Mei 2024 kuwa Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI nchini Tanzania.

**Dkt Lyabwene M. Mtahabwa**

Kamishna wa Elimu

© Tanzania Islamic Studies Association (TISTA)
Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

Toleo la 2024

ISBN: 978-9912 - 992-36-8

Tanzania Islamic Studies Association (TISTA)
Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania
S.L.P 55104,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 7842 67 762
Barua pepe: islamicstudies@tista.or.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Tanzania Islamic Studies Association (TISTA) (2024). Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari, Kidato cha V – VI.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Tanzania Islamic Studies Association (TISTA).

## Yaliyomo


Orodha ya Majedwali……………………………………………………………………iv

Vifupisho…………………………………………………………................…………….. v

Shukurani…………………………………………………….................…………… vi

1.0 Utangulizi ………………………………..…………………………………….. 1

2.0 Malengo makuu ya elimu Tanzania …………..…..............……………………….. 2

3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI ……..….............………… 3

4.0 Malengo ya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI …………………………………………………….............… 3

5.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI ..…..............……. 3

6.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ……..………………………...............… … 4

7.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/ Mlezi katika mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji ………………………………………….......................…… 5

7.1 Mwalimu…………………………………………………........…………… 5

7.2 Mwanafunzi ………………………...…………………………….………… 6

7.3 Mzazi/Mlezi ………………………..….........………………………… 6

8.0 Mbinu zinazopendekezwa za Ufundishaji na Ujifunzaji ……...............……..….. 6

9.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa ………..............……. 6

10.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ……….………...............…………. 6

11.0 Idadi ya Vipindi ………………………………….…...............……….. 7

12.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ……….…………………...............…… 7

Kidato cha V ……………………….………………………...............……….. 8

Kidato cha VI ……………………………………….................…………… 19

Bibliografia ……………………………………………………................….…… 30

**Orodha ya Majedwali**

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi …….............………………... 4

Jedwali Na. 2: Mgawanyo wa Alama za upimaji Endelevu na Tamati …................... 7

Jedwali Na. 3: Maudhui ya Kidato cha Tano ………………….............…………… 8

Jedwali Na. 4: Maudhui ya Kidato cha Sita ………………….............…………… 20

## Vifupisho

A.S: Alayhi Salaam (Juu yake Amani)

IEP: Islamic Education Panel

LAT: Lugha ya Alama ya Tanzania

S.A.W: Swallallahu ‘Alayhi Wasallam (Rehema na Amani za Allaah ziwe juu yake)

S.W: Subhaanahu Wata’ala (Mtukufu Aliye juu)

TEHAMA: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

TET: Taasisi ya Elimu Tanzania

TISTA: Tanzania Islamic Studies Teaching Association

JUMAKITA: Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania

WyEST: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

NECTA: National Examination Council of Tanzania

BAKWATA: Baraza Kuu la Waislamu wa Tanzania

TISOA: Tanzania Integrated School Owners Association

EDK: Elimu ya Dini ya Kiislamu


## Shukurani

Awali ya yote, nielekeze shukurani zangu zisizo na kifani kwa Allah (S.W), Muumba na Mlezi wa viumbe vyote, kwa taufiki yake muhtasari huu umekamilika. Pia, sala na salamu ziende kwa mjumbe wake wa mwisho, Muhammad (S.A.W) pamoja na jamaa, sahaba na umma wake uliomfuata kwa wema.

Shukurani za pekee zimwendee Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara unaolenga kuleta mabadiliko chanya ya elimu, maadili na ustawi mzima wa taifa letu pendwa la Tanzania. Ikumbukwe kuwa kupitia falsafa ya Dkt. Samia ya R4; *Reconciliation* (maridhiano), *Resilience* (ustahamilivu), *Reform* (mabadiliko) na *Rebuilding* (kujenga upya), Tanzania imefanikiwa kuimarika katika nyanja zote za maisha ikiwemo elimu kwa muktadha huu. Yaani, kauli-mbiu yake ya 'Kazi Iendelee' inayosimamiwa na kuongozwa na misingi minne ya falsafa hii, ndio matokeo ya muhtasari huu wa kidato cha tano na sita. Bila shaka, falsafa hii inaashiria mafanikio ya awamu hii katika kulinda, kutetea na kuendeleza amani ya taifa kwa kuendeleza mshikamano, upendo, kuvumiliana kinchi, kikanda na kiduniani kwa ujumla. Kwa msingi huohuo, niishukuru Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kufuata miongozo na maelekezo ya mheshimiwa Rais na kuipa dhamana *Tanzania Islamic Studies Teaching Association* (TISTA) au kwa tafsiri ya Kiswahili Jumuiya ya Ufundishaji wa Masomo ya Kiislamu Tanzania (JUMAKITA), chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mufti wa Tanzania na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar.

Aidha, shukurani nyingine ziende kwa uongozi wa Vyuo Vikuu, Vyuo vya Kati, Shule za Sekondari na taasisi nyingine za Kiislamu kwa kuwaruhusu wataalamu wake kuunga mkono maandalizi ya muhtasari huu. Kadhalika, nilishukuru jopo lililoandaa muhtasari huu, kwani limetendea haki jukumu walilopewa. Jopo hilo liliundwa na Mwl. Shafii Hussein Masudi kutoka Chuo cha Ualimu Ubungo Islamic, Mwl. Mfaume Hamis Nzogera kutoka Chuo cha Ualimu Korogwe, Sheikh Ali Muombwa Hassan kutoka Ofisi ya Mufti Mkuu Zanzibar, Dkt. Nawaje Ali Mganga kutoka Chuo Kikuu cha Abdurahaman Al-Sumait, Dkt. Abdallah Yahya Tego kutoka Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, Dkt. Mohamed Shaibu Same kutoka Chuo cha Kiislamu Zanzibar, Mwl. Ally Nassoro Mohamed kutoka NECTA, Mwl. Said Rajabu Mangi kutoka Ubungo Islamic High School, Mwl. Adam Salim Kaoneka kutoka Chuo cha Ufundi Al-Maktoum, Mwl. Swabrudin Burhani Tibiita kutoka Bagamoyo Professional College, Mwl. Khamis Ali Mohammad kutoka BAKWATA, Mwl. Ally Abdallah Ally kutoka BAKWATA, Mwl. Mwinyikombo Ayubu Akida kutoka TISOA, Imamu Suleimani Daud Mwakanyamale kutoka Masjid Taqwa Mwananyamala. Shukurani nyingine ziwaendee wabobezi wa fani tofauti waliotoa maelekezo na miongozo kutokana na tahasusi zao kwa kuwa Elimu ya Dini ya Kiislamu imekusanya fani mbalimbali ambapo isingewezekana kwa mtu mmoja kutosheleza pasi na kuwa na jopo pamoja na ushauri wa wadau wa somo husika. Hao walishauri na kutoa data kutokana na fani zao zilizosaidia kufanikisha ukamilifu wa muhtasari huu.

Namalizia kwa kuishukuru *Islamic Educational Panel* (IEP), watangulizi wa uandishi wa mihutasari ya Elimu ya Dini ya Kiislamu Tanzania, kwani kupitia mihutasari yao jopo lilipata pa kurejelea. Kwa jumla, nikiri kuwa kuna wengine sitaweza kuwataja kwa majina. Jopo lilishirikiana nao katika kufanikisha muhtasari huu. Nawashukuru wote kwa hilo, Mola Mlezi awalipe kheri.



**Sheikh, Dkt. Abubakar Zubeir bin Ally Mbwana,**
**Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania,**
**Kiongozi Mkuu wa JUMAKITA (TISTA).**

## 1.0 **Utangulizi**

Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu ni moja ya masomo chaguzi katika Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI kwa wanafunzi walio katika mkondo wa elimu ya jumla. Miongoni mwa tahasusi za EDK ni *Islamic Knowledge, History and Geography* (IHG), *Islamic Knowledge, History and Arabic* (IHAr), *Islamic Knowledge, History and English Language* (IHL), *Islamic Knowledge, History and Kiswahili* (IHK), Economics, Business Studies and Islamic Knowledge (EBuI), *Islamic Knowledge, Kiswahili and Arabic* (IKAr), *Islamic Knowledge, Kiswahili and English Language* (IKL). Kimtiririko, wahitimu wa tahasusi hizo wanatarajiwa kujikita au kujiendeleza katika kada za:

1. Ualimu, Akiolojia, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu
2. Ualimu, Akiolojia, Ukalimani na Tafsiri, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu
3. Ualimu, Akiolojia, Ukalimani na Tafsiri, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu
4. Ualimu, Akiolojia, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu
5. Ualimu, Uchumi, Biashara, Uhasibu, Ugavi, Mipango, Uandishi wa Habari, Uhusiano wa Umma, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu.
6. Ualimu, Akiolojia, Ukalimani na Tafsiri, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu
7. Ualimu, Akiolojia, Ukalimani na Tafsiri, Uandishi wa Habari, Rasilimaliwatu, Ukutubi, Utunzaji wa Kumbukumbu

Muhtasari huu ni matokeo ya mapitio ya mihtasari tangulizi katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Tanzania kwa ngazi za kidato cha tano na sita, iliyofanyika katika miaka ya 1982, 1996, 2007 na 2012. Kwa mantiki hiyo, muhtasari huu umejumuisha mazuri yote ya mihtasari tangulizi na kuingiza mambo mapya yanayoafikiana na mapitio ya sera na maboresho ya mitaala Tanzania, yanayolenga kuandaa wahitimu wenye maarifa, mwelekeo, maadili na ujuzi unaoakisi mahitaji halisi katika taifa letu na kuweza kushindana na kushiriki kikamilifu katika soko la ajira duniani. Pia, yamezingatia masuala muhimu yanayopewa kipaumbele katika dunia kama vile mabadiliko ya tabia-nchi, elimu kuhusu Uraia wa Dunia na Stadi za Karne ya 21 kama ilivyobainishwa na Waraka wa Elimu Na. 05 wa Mwaka 2023 kuhusu Utekelezaji wa Mitaala Iliyoboreshwa. Hayo yote yamenasibishwa na miongozo ya Qur'an na Sunnah kwa kuwa ndiyo misingi na marejeleo makuu ya dini ya Kiislamu.

Maandalizi ya muhtasari huu yameshirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wanafunzi wa vyuo vikuu, vyuo vya kati, na sekondari; wahadhiri, wakufunzi, na walimu kutoka vyuo vikuu, vya kati, na shule za sekondari za umma na binafsi; viongozi wa kisiasa; wazazi na walezi; viongozi wa Serikali, viongozi wa Dini, wakuu wa taasisi za elimu, wathibiti ubora wa elimu, mashirika mbalimbali na asasi za kiraia. Lengo ni kuleta uelewa wa pamoja na kujumuisha mawazo na maoni ya wadau wote wa EDK.

Lugha ya kufundishia, Kiswahili kitatumika kufundishia EDK kwa ngazi hii badala ya Kiingereza kama ilivyokuwa awali. Hii inatokana na ruhusa iliyotolewa na waraka tajwa hapo juu, maoni yaliyotolewa na wadau wa EDK na mahitaji ya somo husika kutilia msisitizo katika itikadi, imani na matendo ili kuwawezesha wahitimu wake kumudu utekelezaji wa makusudio ya somo katika maisha ya kila siku. Ifahamike kwamba nchi bila ya maadili haina amani, wakati amani haipatikani kwa mtutu wa bunduki bali kwa kuzitengeneza nafsi na nyoyo za raia. Nyoyo hizo, hazitengezwi hospitali wala kwa fundi yeyote yule, ni elimu ya kiroho tu ndiyo yenye nafasi hiyo. Hivyo, ni wakati mwafaka sasa somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu kufundishwa kwa lugha inayoeleweka zaidi ili kuleta athari inayokusudiwa kwa mustakabali mwema wa taifa letu.

Muhtasari huu umejikita katika umahiri mkuu wa aina nne, na kila umahiri mkuu una umahiri mahsusi; (1) **Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu** (Kuchambua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu, Kuthibitisha usahihi wa Itikadi ya Uislamu, na Kuthamini nguzo za Imani ya Kiislamu), (2) **Kuthamini Qur'an na Sunnah** (Kuthibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah (S.W), Kuchambua misingi ya kufasiri Qur'an, Kuthibitisha usahihi wa Sunnah, na Kuchambua mambo mtambuka katika jamii kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah), (3) **Kumtumikia Allah (S.W) katika nyanja zote za maisha** (Kutathmini utekelezaji wa nguzo za Uislamu, Kutathmini mifumo ya maisha kwa mujibu wa Uislamu, Kufafanua misingi ya Sharia, Kuthamini matumizi ya Sharia katika miamala mbalimbali), (4) **Kuthamini historia katika kuimarisha Haki na uadilifu katika jamii** (Kufafanua dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu, Kutathmini historia ya Uislamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) hadi hivi sasa, na Kujenga mwenendo mwema wa jamii).

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu nchini Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, na mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda tunu za taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia na usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI

Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI ni:

(a) Kuimarisha, kupanua na kuendeleza uelewa wa kina wa maarifa, stadi, na mwelekeo alioupata katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Kidato cha I–IV;
(b) Kulinda mila na desturi, tunu za taifa, demokrasia na kuthamini haki za binadamu na za kiraia, na wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;
(c) Kukuza tabia ya kujiamini na uwezo wa kujifunza kwenye nyanja mbalimbali zikiwemo sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, na kiufundi;
(d) Kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;
(e) Kuimarisha uwajibikaji katika masuala mtambuka ya kijamii, yakiwemo afya, usalama, usawa wa kijinsia, na utunzaji endelevu wa mazingira;
(f) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na
(g) Kumwandaa mwanafunzi kujiunga na vyuo vya kati na elimu ya juu.

## 4.0 Malengo ya somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI

Mwanafunzi anayesoma somo hili, baada ya kumaliza kidato cha Sita anatarajiwa amudu:

(a) Kuthibitisha kivitendo itikadi sahihi ya Kiislamu
(b) Kutathmini utekelezaji wa nguzo za Uislamu katika maisha
(c) Kuthibitisha Sharia katika miamala mbalimbali
(d) Kuthamini mafunzo ya Qur’an katika maisha ya kila siku
(e) Kutathmini historia ya Uislamu katika kuimarisha haki na uadilifu katika jamii.
(f) Kuthamini mafunzo ya Sunnah na Hadith katika maisha ya kila siku
(g) Kukuza utayari wa kujiendeleza kielimu katika ngazi ya juu.

## 5.0 Umahiri wa Jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V – VI

Umahiri wa jumla wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V –VI ni:

(a) Kutumia maarifa na stadi alizozipata katika ngazi ya Elimu ya Sekondari Hatua ya Chini kuimarisha na kupanua uelewa wake kitaaluma;
(b) Kuthamini uraia, tunu za taifa, na haki za binadamu na za raia;
(c) Kujiamini katika ujifunzaji wa nyanja mbalimbali zikiwemo, sayansi na teknolojia na maarifa ya kinadharia na kivitendo;
(d) Kutumia stadi za lugha katika mawasiliano ya kitaaluma;

(e) Kutumia maarifa ya masuala mtambuka ili kumudu mazingira yanayomzunguka;

(f) Kutumia ujuzi na stadi alizozipata kumwezesha kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake; na

(g) Kuonesha utayari wa kujiunga na ngazi ya elimu inayofuata.

## 6.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotakiwa kujengwa kwa Kidato cha V–VI umebainishwa katika jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Kidato cha V – VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu | 1.1 Kuchambua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu<br>1.2 Kuthibitisha usahihi wa Itikadi ya Uislamu<br>1.3 Kuthamini nguzo za Imani ya Kiislamu |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na Sunnah | 2.1 Kuthibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah (S.W)<br>2.2 Kuchambua misingi ya kufasiri Qur'an<br>2.3 Kuchambua dhana ya Sunnah<br>2.4 Kuchambua mambo mtambuka katika jamii kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah |
| 3.0 Kumtumikia Allah (S.W) katika nyanja zote za maisha | 3.1 Kutathmini utekelezaji wa nguzo za Uislamu<br>3.2 Kutathmini mifumo ya maisha kwa mujibu wa Uislamu<br>3.3 Kufafanua misingi ya Sharia<br>3.4 Kuthamini matumizi ya Sharia katika miamala mbalimbali |
| 4.0 Kuthamini historia katika kuimarisha Haki na Uadilifu katika jamii | 4.1 Kufafanua dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu<br>4.2 Kutathmini historia ya Uislamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) hadi hivi sasa<br>4.3 Kujenga mwenendo mwema wa jamii |

## 7.0 Majukumu ya Mwalimu, Mwanafunzi na Mzazi/ Mlezi katika mchakato wa Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano madhubuti baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi katika kutekeleza majukumu mbalimbali. Majukumu hayo ni kama yafuatayo:

### 7.1 Mwalimu

Mwalimu anatarajiwa:

(a) Kumwezesha mwanafunzi kujifunza na kupata umahiri uliokusudiwa katika somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu;

(b) Kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia zitakazomwezesha mwanafunzi:

(i) Kujenga umahiri unohitajika katika Karne ya 21; na

(ii) Kushiriki ipasavyo katika tendo zima la ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wa mwanafunzi.

(c) Kutumia mbinu shirikishi zinazomfanya mwanafunzi kuwa kitovu cha ujifunzaji zikiwemo zile zitakazomwezesha mwanafunzi kufikiri, kutafakari na kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Mbinu za kufundishia na kujifunzia zinazopendekezwa ni pamoja na kazi za vitendo, utafiti, majadiliano na kazimradi zinazolenga kutatua matatizo halisi katika mazingira ya mwanafunzi. Aidha mwalimu anahimizwa kutumia njia nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujenzi wa umahiri uliokusudiwa.

(d) Kuandaa darasa salama lenye mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia;

(e) Kutengeneza au kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia;

(f) Kufanya upimaji endelevu mara kwa mara kwa kutumia zana na mbinu za upimaji na tathmini zinazopima nadharia na vitendo zikiwemo bunguabongo, orodhahakiki, majaribio, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi, kazi za vikundi), kazimradi na mkoba wa kazi. Zana na mbinu nyingine ni majaribio kwa vitendo, uwasilishaji, mitihani ya muhula na mtihani wa mwisho;

(g) Kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa haki na usawa kwa kila mwanafunzi bila kujali tofauti zao;

(h) Kumlinda mwanafunzi awapo shuleni;

(i) Kufuatilia maendeleo ya mwanafunzi ya kila siku;

(j) Kubaini mahitaji ya kila mwanafunzi na kutoa afua stahiki;

(k) Kushirikisha wazazi/walezi na jamii katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa mwanafunzi; na

(l) Kutomea masuala mtambuka na TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

7.2 **Mwanafunzi**

Mwanafunzi anatarajiwa:

(a) Kuwa mtendaji mkuu katika mchakato wote wa ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujifunzaji ndani na nje ya darasa ili kupata umahiri unaokusudiwa; na

(c) Kushiriki katika kutafuta maarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo vitabu vya kiada, ziada na machapisho mengine kutoka katika maktabamtandao.

**7.3 Mzazi/Mlezi**

Mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia maendeleo ya mtoto katika ujifunzaji;

(b) Kumsimamia mtoto kutekeleza kazi zake za kitaaluma pale inapowezekana;

(c) Kuhakikisha kuwa mazingira ya nyumbani ni rafiki na salama yanayowezesha ujifunzaji

(d) Kufuatilia mwenendo na tabia ya mtoto;

(e) Kumpatia mtoto vifaa vyote vinavyohitajika katika ujifunzaji;

(f) Kuhakikisha mwanafunzi anapata mahitaji muhimu; na

(g) Kumfundisha mtoto kuhusu umuhimu na thamani ya elimu pamoja na kumhimiza kujifunza kwa bidii.

**8.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji**

Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji ni msingi katika kujenga umahiri kwa mwanafunzi. Muhtasari huu unapendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa kila shughuli. Miongoni mwa mbinu hizo ni changanyakete, kazimradi na kazi za vitendo. Hata hivyo mwalimu anashauriwa kutumia mbinu nyingine kama hizo kulingana na muktadha wa ujifunzaji.

**9.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji Zinazopendekezwa**

Mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unahitaji zana mbalimbali ili kujenga umahiri uliokusudiwa. Hivyo, mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kushirikiana katika kuandaa au kufaragua zana zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na nyumbani pindi vinapohitajika. Mwalimu na mwanafunzi wanapaswa kutafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kuleta ufanisi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

**10.0 Upimaji**

Upimaji ni mchakato muhimu katika ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Elimu ya Dini ya Kiislamu. Mwalimu anashauriwa kuwa na uwanja mpana wa uchaguzi wa mbinu na zana za upimaji ili kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuchambua na

kutafsiri Qur’an na Hadith, kuchambua historia ya Uislamu, kuandaa mipango ya kuendeleza Uislamu na kutekeleza ibada mbalimbali kwa usahihi. Aidha, upimaji utahusisha upimaji endelevu na upimaji tamati. Upimaji endelevu utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji na utamwezesha mwalimu kubaini uwezo na mahitaji ya mwanafunzi katika ujifunzaji. Zana za upimaji zinazoweza kutumika wakati wa ufundishaji na ujifunzaji ni bunguabongo, orodhahakiki, mazoezi ya darasani, majaribio, majaribio kwa vitendo, dodoso, maswali ya ana kwa ana, mazoezi, kazi kwa vitendo (kazi binafsi na kazi za vikundi), mkoba wa kazi na zana nyingine kama hizo. Hivyo, upimaji endelevu utachangia asilimia 30 ya upimaji wote na upimaji kitaifa wa kuhitimu Kidato cha VI utachangia asilimia 70. Mchanganuo wa upimaji endelevu na kitaifa umebainishwa katika Jedwali Na. 2.

Jedwali Na.2: *Mgawanyo wa Alama za Upimaji Endelevu na Kitaifa*

| **Upimaji** | **Alama(%)** |
|---|---|
| Mtihani wa muhula wa kwanza kidato cha V | 5 |
| Mtihani wa muhula wa pili kidato cha V | 5 |
| Mtihani wa muhula wa kwanza kidato cha VI | 5 |
| Kazimradi | 10 |
| Mtihani wa utamilifu kidato cha VI | 5 |
| Mtihani wa Taifa wa Kidato cha VI | 70 |
| **Jumla** | **100** |

## 11.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za ujifunzaji. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 40. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni kumi (10) kwa wiki kwa kidato cha V–VI.

## 12.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele saba ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, mbinu zinazopendekezwa, vigezo vya upimaji, zana pendekezwa, na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

## Kidato cha V

**Jedwali Na.3:** *Maudhui ya Kidato cha V*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu | 1.1 Kuchambua dhana ya Elimu kwa mtazamo wa Uislamu | (a) Kutofautisha maana na malengo ya elimu baina ya Uislamu na itikadi nyingine | **Fikiri – Andika – Jozisha – Shirikisha:** Waongoze wanafunzi katika jozi kujadili tofauti za kimaana na malengo ya elimu baina ya Uislamu na itikadi nyingine | Maana na malengo ya elimu baina ya Uislamu na itikadi nyingine yametofautishwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, Tafsir ya Riyadhus Salihina, matini mbalimbali kuhusu elimu | 10 |
| | | (b) Kubainisha nafasi na umuhimu wa elimu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi kujadili katika vikundi nafasi na umuhimu wa elimu kisha wawasilishe | Nafasi na umuhimu wa elimu umebainishwa | | 10 |
| | | (c) Kubainisha dhana potofu kuhusu elimu na athari zake | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kudadisi dhana potofu kuhusu elimu kwa kuulizana maswali kisha kuwasilisha<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili athari za mitazamo potofu juu ya elimu | Dhana potofu kuhusu elimu na athari zake imebainishwa | | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (d) Kuchambua mchango wa Waislamu katika fani za sayansi na teknolojia | **Utafiti mdogo:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kufanya utafitimdogo kuhusu mchango wa Waislamu katika fani za sayansi na teknolojia kisha kuwasilisha | Mchango wa Waislamu katika fani za sayansi na teknolojia umechambuliwa | | 18 |
| | 1.2 Kuthibitisha usahihi wa Itikadi ya Uislamu. | (a) Kubainisha tofauti kati ya itikadi ya Uislamu na itikadi nyingine na athari zake | **Utafiti mdogo:**<br><br>Waongoze wanafunzi kutafiti tofauti za kiitikadi kati ya Uislamu, Ushirikina, ukafiri na utawa | Tofauti kati ya itikadi ya Uislamu na itikadi nyingine na athari zake imebainishwa | Kitabu cha kiada kidato cha V,<br>Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu itikadi mbalimbali | 18 |
| | 1.3 Kuthamini nguzo za Imani ya Kiislamu | (a) Kuchambua nguzo za Imani | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi wabainishe dhana ya Uungu kwa kupitia maswali na majibu.<br><br>**Ziara ya kimafunzo:** Waongoze wanafunzi kufanya ziara ya kimafunzo kwenda kutafakari uumbaji wa | Nguzo za imani zimechambuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha V,<br>Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu Imani ya Kiislamu | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Allah (S.W) kama vile milima, vyanzo vya maji, wanyama, mazao, wadudu na miji ya kihistoria.<br><br>**Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kuchambua hoja zinazothibitisha kuwa kumuamini Allah (S.W) si suala la kibubusa | | | |
| | | (b) Kupambanua athari za nguzo za Imani katika maisha | **Changanyakete:** Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili kuhusu athari za kumuamini Allah (S.W), Malaika, Vitabu, Mitume, Siku ya mwisho na Qadar kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho. | Athari za nguzo za Imani katika maisha zimeng'amuliwa | | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kuthamini Qur'an na Sunnah | 2.1 Kuthibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah (S.W) | (a) Kuchambua hoja potofu zinazoelezwa dhidi ya Qur'an | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi kusoma na kuchambua hoja za wapinzani wa Qur'an wa kale na sasa.<br>**Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili matendo ya wapinzani dhidi ya Qur'an na athari zake. | Hoja potofu zinazoelezwa dhidi ya Qur'an zimechambuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu Qur'an | 18 |
| | | (b) Kuonesha hoja zinazothibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah (S.W) | **Kazimradi:** Wagawe wanafunzi katika vikundi kisha wape jukumu la kuandaa kazimradi kuhusu historia ya kuhifadhiwa kwa Qur'an<br>**Changanyakete:** Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili hoja zinazothibitisha kuwa Qur'an ni maneno ya Allah kupitia:<br>(i) Mtume Muhammad (S.A.W) | | | 14 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (ii) Maudhui ya Qur'an<br>(iii) Lugha ya Qur'an<br>(iv) Historia ya kushuka na kuhifadhiwa kwa Qur'an<br>Kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jingine kufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho. | | | |
| | 2.2 Kuchambua misingi ya kufasiri Qur'an | (a) Kufafanua dhana ya tafsiri ya Qur'an | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili maana, malengo na historia ya kufasiri Qur'an. Pia, kutofautisha baina ya tafsiri na *taawil* | Dhana ya tafsiri ya Qur'an imefafanuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Ibn Abbas, Twabari Ibn Kathir, Tafsir ya Qur'an ya Jalalain, Tafsir ya Qur'an ya Fidhilalil Qur'an na Tafhimul Qur'an, matini mbalimbali kuhusu Qur'an | 6 |
| | | (b) Kufafanua ngazi za tafsiri ya Qur'an | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi waeleze misingi ya Tafsir *maathur* na *tafsir* ya rai kutokana na matini teule | Ngazi za tafsiri ya Qur'an zimefafanuliwa | | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kufafanua dhana ya *Sababun Nuzul* katika kufasiri Qur'an | **Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa kufasiri Qur'an ili afafanue dhana ya *Sababun Nuzul* katika kufasiri Qur'an<br>**Midia anuai:**<br>Waongoze wanafunzi kusikiliza au kutazama tafsiri ya Qur'an inayozungumzia *Sababun Nuzul* | Dhana ya *Sababun Nuzul* katika kufasiri Qur'an imefafanuliwa | | 8 |
| | | (d) Kufafanua masharti ya mfasiri wa Qur'an | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili masharti ya mfasiri Qur'an | Masharti ya mfasiri Qur'an yamefafanuliwa | | 8 |
| | | (e) Kubainisha dhana ya *Nasikh* na *Mansukh* | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili dhana ya Nasikh na Mansukh | Dhana ya Nasikh na Mansukh imebainishwa | | 6 |
| | 2.3 Kuchambua dhana ya Sunnah | (a) Kuchambua hoja potofu zinazonasibishwa na Sunnah | **Maswali na majibu:**<br>Waongoze wanafunzi wabainishe maana, aina na hoja potofu za kimaana na kimatumizi zinazonasibishwa na Sunnah kupitia maswali na majibu | Hoja potofu zinazonasibishwa na Sunnah zimechambuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha V,<br>Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu Sunnah | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kuchambua hoja za ukubalifu wa Hadithi | **Kazimradi:** Wagawe wanafunzi katika vikundi kisha wape jukumu la kuandaa kazimradi kuhusu kuchambua usahihi wa hadithi kwa mujibu wa matini na isnad | Hoja za ukubalifu wa Hadithi zimechambuliwa | | 10 |
| | | (c) Kubainisha umuhimu wa kutekeleza Sunnah | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili umuhimu wa kutekeleza Sunnah | Umuhimu wa kutekeleza Sunnah imebainishwa | | 10 |
| 3.0 Kumtumikia Allah (S.W) katika nyanja zote za maisha | 3.1 Kutathmini utekelezaji wa nguzo za Uislamu. | (a) Kuonesha kutegemeana kwa nguzo za Uislamu katika utekelezaji wake | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi kudadisi kuhusu kutegemeana kwa nguzo za Uislamu katika utekelezaji wake kwa kuulizana maswali kisha kuwasilisha | Kutegemeana kwa nguzo za Uislamu katika utekelezaji wake kumeoneshwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, Tafsir ya Riyadhus Salihina, matini mbalimbali kuhusu nguzo za Uislamu | 10 |
| | | (b) Kubainisha masharti na matendo ya nguzo za Uislamu yanavyofanikisha malengo yake | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili masharti na matendo ya nguzo za Uislamu yanavyofanikisha malengo yake | Masharti na matendo ya nguzo za Uislamu yanavyofanikisha malengo yake yamebainishwa | | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 3.2 Kutathmini mifumo ya maisha kwa mujibu wa Uislamu | (a) Kubainisha dhana ya mfumo wa maisha | **Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi wabainishe dhana ya mfumo wa maisha kupitia maswali na majibu | Dhana ya mfumo wa maisha imebainishwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, Tafsir ya Riyadhus Salihina, matini mbalimbali kuhusu mifumo ya maisha | 8 |
| | | (b) Kujadili mifumo ya maisha iliyopo na athari zake | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili misingi ya mifumo ya maisha ya Ubepari, Ujamaa na Uislamu kisha wabainishe athari za mifumo hiyo | Mifumo ya maisha iliyopo na athari zake imejadiliwa | | 20 |
| | | (c) Kuthibitisha mfumo sahihi anaostahiki mwanadamu kuufuata | **Kazimradi:** Wagawe wanafunzi katika vikundi kisha wape jukumu la kuandaa kazimradi kuhusu kuthibitisha mfumo sahihi anaostahiki mwanadamu kuufuata<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili | Mfumo sahihi anaostahiki mwanadamu kuufuata umethibitishwa | | 8 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | unyumbufu wa Uislamu kwa mujibu wa miktadha | | | |
| 4.0 Kuthamini historia katika kuimarisha Haki na Uadilifu katika jamii | 4.1 Kufafanua dhana ya Historia kwa mujibu wa Uislamu | (a) Kubainisha dhana ya historia katika Uislamu | **Bungua bongo:** Waongoze wanafunzi wabainishe dhana ya historia katika Uislamu kwa kuulizana maswali na kisha kuwasilisha | Dhana ya historia katika Uislamu imebainishwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu historia | 8 |
| | | (b) Kufafanua historia ya mwanadamu | **Bunguabongo:** Waongoze wanafunzi wafafanue mkataba wa awali waliochukua wanadamu mbele ya Mola wao kwa kuulizana maswali na kisha kuwasilisha<br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili historia ya mwanadamu kwa kuzingatia asili, lengo, hadhi na dhima yake. | Historia ya mwanadamu imefafanuliwa | | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 4.2 Kutathmini historia ya Uislamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) hadi hivi sasa | (a) Kufafanua historia ya maisha ya mwanadamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) | **Changanyakete:** Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili historia ya maisha ya mwanadamu kiuchumi, kisiasa, kiteknolojia na kijamii kupitia Manabii waliotangulia kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jinginekufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho | Historia ya maisha ya mwanadamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) imefafanuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu historia | 20 |
| | | (b) Kufafanua ustawi wa Uislamu wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W) | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili: (i) Njia alizotumia Mtume Muhammad (S.A.W) kufikisha ujumbe na hekima zake (ii) Namna Mtume Muhammad (S.A.W) alivyoandaa ummah (iii) Mbinu za makafiri dhidi ya Uislamu na namna Mtume Muhammad (S.A.W) na Waislamu walivyokabiliana nazo | Ustawi wa Uislamu wakati wa Mtume Muhammad (S.A.W) umefafanuliwa | | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kubainisha ustawi wa Uislamu wakati wa Makhalifa waongofu | **Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili:<br>(i)Taratibu za kupatikana viongozi na mafunzo yatokanayo<br>(ii)Mbinu za kiuongozi<br>(iii)Maendeleo ya kimiundo mbinu<br>(iv)Mifumo ya jeshi, ulinzi na usalama<br>**Changanyakete:**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili mifumo ya uchumi, mbinu za da'awa na kuibuka kwa fitina na madhara yake kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jinginekufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho | Ustawi wa Uislamu wakati wa Makhalifa waongofu umebainishwa | | 18 |

## Kidato cha VI

**Jedwali Na.4:** *Maudhui ya Kidato cha VI*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kuishi kwa mujibu wa itikadi ya Uislamu | 1.2 Kuthibitisha usahihi wa itikadi ya Uislamu | (a) Kuchambua uhusiano wa kiitikadi baina ya Uislamu na itikadi nyingine | **Matembezi ya galari:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mambo yanayofaa kushirikiana na mambo yasiyofaa kushirikiana baina ya itikadi ya Uislamu na itikadi nyingine na kuyaandika kwenye manila au karatasi kubwa na kuzibandika, ili wanafunzi katika makundi wazunguke wakisoma na kujadili. | Uhusiano wa kiitikadi baina ya Uislamu na itikadi nyingine umechambuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu itikadi | 10 |
| | | (b) Kuonesha kuwa Uislamu ni dini anayostahiki kuifuata mwanadamu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili vigezo vya dini sahihi.<br><br>**Maswali na majibu:** Waongoze wanafunzi waoneshe namna Uislamu unavyokidhi vigezo vya dini | Imeoneshwa kuwa Uislamu ni dini anayostahiki kuifuata mwanadamu | | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kuthamini nguzo za Imani ya Kiislamu | (a) Kuchambua nguzo za Imani | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili:<br>(i) Kategoria ya nguzo za Imani kwa kuzingatia aya husika za Qur'an<br>(ii)Uhusiano wa nguzo za imani namna zinavyo tegemeana na kukamilishana | Nguzo za imani zimechambuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu nguzo za Imani na nguzo ya Ihsan | 20 |
| | | (b) Kufafanua nguzo ya Ihsan | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi wajadili katika vikundi namna ya kuitekeleza nguzo ya ihsan. | Nguzo ya Ihsan imefafanuliwa | | 10 |
| 2.0 Kuthamini Qur'an na Sunnah | 2.4 Kuchambua mambo mtambuka katika jamii kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. | (a) Kufafanua mwongozo wa Uislamu kuhusu mambo mtambuka | **Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa mambo mtambuka ili afafanue yanayozingatiwa na Uislamu katika kutoa mwongozo kuhusu mambo mbalimbali yanayoibuka katika jamii kulingana na zama na mahali. | Mwongozo wa Uislamu kuhusu mambo mtambuka umefafanuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu mambo mtambuka | 10 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili namna ambavyo Qur'an inavyojithibitisha kuwa haipitwi na wakati | | | |
| | | (b) Kuchambua mambo mtambuka | **Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa jambo mtambuka unalokusudia kufundisha ili alifafanue jambo hilo<br><br>**Midia anuai:**<br>Waongoze wanafunzi kusikiliza au kutazama mambo mtambuka | Mambo mtambuka yamechambuliwa | | 20 |
| 3.0 Kumtumikia Allah (S.W) katika nyanja zote za maisha | 3.3 Kufafanua misingi ya Sharia | (a) Kueleza dhana ya *Maqasid sharia* | **Bunguabongo:**<br>Waongoze wanafunzi waeleze maana ya sharia na makusudio yake kwa kuulizana maswali na kisha kuwasilisha | Dhana ya *Maqasid sharia* imeelezwa | Kitabu cha kiada kidato cha V, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (b) Kubainisha matumizi ya misingi ya kiada na ziada ya sharia | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili:<br>(i) Matumizi ya misingi ya kiada na ziada ya sharia<br>(ii) Msingi wa halali na haramu katika Uislamu | Matumizi ya misingi ya kiada na ziada ya sharia imebainishwa | Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu sharia | 28 |
| | | (c) Kubainisha uthabiti wa sharia na unyumbufu wa fat-wa na rai | **Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa sharia ili abainishe uthabiti wa sharia na unyumbufu wa fat-wa na rai | Uthabiti wa sharia na unyumbufu wa fat-wa na rai umebainishwa | | 18 |
| | 3.4 Kuthamini matumizi ya Sharia katika miamala | (a) Kubainisha mfumo wa kiuchumi katika Uislamu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili dhana ya uchumi katika Uislamu kwa kuangalia maana, misingi na vyanzo vya mali, nidhamu ya biashara katika Uislamu<br><br>**Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa mifumo ya kibenki ili atoe uzoefu kuhusu ujuzi huo. | Mfumo wa kiuchumi katika Uislamu umebainishwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu sharia za muamala | 40 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Ziara ya kimafunzo:**<br>Waongoze wanafunzi kufanya ziara ya kimafunzo kwenda kwenye taasisi zinazotoa huduma za mfumo wa *takaful* na mfumo wa wakfu<br>**Uchambuzi wa matini:**<br>Waongoze wanafunzi wabainishe mfumo wa *takaful* na mfumo wa wakfu kutokana na matini za muamalat | | | |
| | | (b) Kufafanua mfumo wa kijamii katika Uislamu | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili mfumo wa familia ya Kiislamu na ujirani.<br>**Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa afya, michezo, misiba na sherehe kwa mujibu wa Uislamu ili afafanue kuhusu ujuzi huo | Mfumo wa kijamii katika Uislamu umefafanuliwa | | 30 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kubainisha mfumo wa kisiasa katika Uislamu | **Changanyakete:** Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili kuhusu uongozi, uraia, uzalendo, utaifa na utandawazi kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jinginekufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho<br>**Kualika mgeni:**<br>Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa mfumo wa siasa afafanue mtazamo wa Uislamu juu ya siasa | Mfumo wa kisiasa katika Uislamu umebainishwa | | 10 |
| | | (d) Kubainisha mfumo wa kielimu katika Uislamu | **Uchambuzi wa matini:** Waongoze wanafunzi wabainishe maendeleo ya elimu katika Uislamu, mifumo ya elimu dhidi ya Uislamu na mitaala kutokana na matini teule | Mfumo wa kielimu katika Uislamu umebainishwa | | 18 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (e) Kufafanua mfumo wa kimahakama katika Uislamu | **Ramani ya dhana:** Andaa ramani ya dhana kuhusu mgawanyo wa makosa katika Uislamu ambapo utajaza baadhi ya vipengele na kuacha vingine ili vijazwe na wanafunzi<br><br>**Kualika mgeni:** Alika mgeni ambaye ana ujuzi wa sharia na sheria ili afafanue mfumo wa uendeshaji wa kesi na utoaji wa hukumu<br><br>**Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili kuhusu taratibu za mahabusu na jela/chuo cha mafunzo | Mfumo wa kimahakama katika Uislamu umefafanuliwa | | 10 |
| 4.0 Kuthamini historia katika kuimarisha Haki na Uadilifu katika jamii | 4.2Kutathmini historia ya Uislamu kabla ya Mtume Muhammad (S.A.W) hadi hivi sasa | (a) Kufafanua ustawi wa Uislamu wakati wa dola ya Banu Umayyah na Banu Abbas | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili ustawi wa Uislamu wakati wa dola ya Banu Umayyah na Banu Abbas kwa kuzingatia mafanikio, changamoto na | Ustawi wa Uislamu wakati wa dola ya Banu Umayyah na Banu Abbas umefafanuliwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | mafunzo yatokanayo<br><br>**Maswali na Majibu:**<br>Waongoze wanafunzi wafafanue mchango wa Umar bin Abdul – Aziz na Harun Rashid katika kuleta ustawi wa Uislamu katika jamii na mafunzo yatokanayo | | Barwan, matini mbalimbali kuhusu historia | |
| | | (b) Kufafanua ustawi wa Uislamu Wakati na Baada ya dola ya Uthmaniyy ah | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili ustawi wa Uislamu wakati wa dola ya Uthmaniyyah kwa kuzingatia mafanikio, changamoto na mafunzo yatokanayo<br><br>**Maswali na Majibu:**<br>Waongoze wanafunzi wafafanue mchango wa Uthmani bin Altoghro na wasomi wengine wa zama hizo katika kuleta ustawi wa | Ustawi wa Wakati na Baada ya dola ya umefafanuliwa | | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Uislamu katika jamii na mafunzo yatokanayo. | | | |
| | | (c) Kufafanua ustawi wa Uislamu Afrika | **Majadiliano:** Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili historia ya kuingia na kuenea kwa Uislamu Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na Afrika Kaskazini kwa kuzingatia mafanikio, changamoto na mafunzo yatokanayo, kisha kila kikundi kiwasilishe mbele ya darasa na wengine wachangie na mwisho utathmini hoja na kufanya majumuisho<br><br>**Uchambuzi wa matini**<br><br>Kwa kutumia matini teule, waongoze wanafunzi kusoma na kuchambua historia Uislamu Afrika Mashariki, Afrika Magharibi na Afrika Kaskazini | Ustawi wa Uislamu Afrika umefafanuliwa | | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Changanyakete:**<br><br>Waongoze wanafunzi katika vikundi wajadili mchango wa Sheikh Suleiman bin Alawy, Sheikh Hassan bin Amir, Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Ali Muhsin Barwan, Mansa Musa, Ahmed Deedat katika kuleta ustawi wa Uislamu katika jamii na mafunzo yatokanayo kisha elekeza kila kundi kutoa mwakilishi mmoja kwenda kundi jinginekufundisha walichojifunza katika kundi lao kisha fanya majumuisho | | | |
| | 4.3 Kujenga mwenendo mwema wa jamii | (a) Kutathmini mbinu za da'awah kulingana na wakati | **Uchambuzi wa matini:**<br><br>Kwa kutumia matini teule, waongoze wanafunzi kusoma na kuchambua mbinu mbalimbali za da'awah kulingana na wakati na muktadha | Mbinu za da'awah kulingana na wakati zimetathminiwa | Kitabu cha kiada kidato cha VI, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Abdullah Saleh Farsy, Tafsir ya Qur'an ya Sheikh Ali Muhsin Barwan, matini mbalimbali kuhusu da'awah | 20 |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Vigezo vya upimaji | Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazo pendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | **Kazimradi:**<br>Wagawe wanafunzi katika vikundi kisha wape miktadha mbalimbali ili waandae mipango kazi ya kiulinganizi<br>**Majadiliano:**<br>Waongoze wanafunzi katika vikundi kujadili changamoto katika da'awah na namna ya kukabiliana nazo kisha kuwasilisha na fanya majumuisho | | | |
| | | (b) Kujihusisha na da'awah | **Kazi mradi:**<br>Waongoze wanafunzi wafanye kazi ya da'awah shuleni kisha kuandika ripoti kuhusu mafanikio, changamoto na namna walivyokabiliana nazo | Wanafunzi wamejihusisha na da'awah | | 18 |

**Bibliografia**

Islamic Education Panel (2012), Islamic knowledge syllabus for secondary school form V – VI. Islamic Education Panel (Dar es Salaam).

Tanzania Islamic Studies Teaching Association (2023) Muhtasari wa Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari Kidato Cha I – IV. Dar es Salaam: TISTA.

Farsy.A.S (1987). Tafsiri ya Kiswahili ya Qur'an Tukufu. The Islamic Foundation (Nairobi, Kenya).

Tafsiri ya Kiswahili ya Riyadhus Salihiin, chapa ya pili (2018). Ibn Hazm Media Center (Dar es Salaam).

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI), (2019) Kamusi ya Kiswahili sanifu, Chuo kikuu cha Dar es Salaam (Dar es Salaam, Tanzania).

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (WyEST), Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la mwaka 2023, Dodoma – Tanzania.

Cambridge International AS & A level, Islamic Studies 9488, For examination in June and November 2021, 2022 and 2023.

Jalaluddin Al – Mahalli and Jalaluddin Al – Suyuti, Tafsir Al – Jalalayn, Translated by Feras Hamza, Royal Aal Bayt Institute for Islamic Thought, Amman – Jordan.

Tafsir ya Ibn Kathir, iliyofasiriwa na kamati ya wataalamu, Ibn Hazm Media Centre – Dar es Salaam, Tanzania.

Ali Muhsin Barwan (1995), Tarjama Al – Muntakhab katika Tafsiri ya Qur'an Tukufu, King Fahd Press: Madinah – Saudi Arabia.